Jina………………………………………………………………. Nambari yako……………../………

Shule…………………………………………………………... Sahihi yako…….……………….....

Tarehe …………………………….…...

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**
**JULY / AGOSTI - 2010**
**MUDA: SAA 2 ½**

# TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI - 2010

***Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (KCSE)***

**102/2**
**KISWAHILI**
Karatasi ya 2
**(LUGHA)**
**JULAI / AGOSTI - 2010**
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

1. Karatasi hii ina maswali **manne**. (Ufahamu, ufupisho, lugha na Isimu Jamii)
2. Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | | |

***Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa***
***Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.***

*© 2010 Halmashuri ya Mtihani Wilaya ya Bureti* 

1. **UFAHAMU**

**Soma makala yafuatavo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Licha ya kuwa na historia ya kiasi, maisha ya binadamu ni kioja kikubwa. Hebu jiulize jinsi uhai wako rnwenyewe ulivyoanza sembuze unavyoweza kupumua na kuishi siku nenda siku rudi.

Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Mungu Muumba. Hata hivyo Muumba hutumia mume na mke kutuanzishia maisha yetu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la mwanamke muda mfupi tu baada ya mke na mume kushirikiana katika tendo la kujamiiana. Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanaume hudunga na kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo, mtu huwa na mama akawa mja mzito. Hatua ya kwanza ya uhai!

Wanasayansi wametuthibitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanaume ina kromosomu ishirini na tatu (23) nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya kromosomu. Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini na sita (46). Kromosomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu na kukadiria mambo mbalimbali adhimu. Kwa mfano, hukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu mweusi, mwerevu au wa akili chache, mwenye nywele za singa au za kipilipili, atakuwa na damu ya namna gani, michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za usoni.

Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga juu ya yaliyokwisha kuanzilishwa na kromosomu katika yai lilitorutubishwa tumboni.

Haihalisi kabisa kufikiria kwamba katika hatua za mwanzo tumboni mwa mama, kiumbe huwa katika hali ya ukupe. La hasha! Yeye hujitegemea kwa vyovyote na ana upekee wake. Hatangamani na mama yake. Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa na ya mama yake, humtembea na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyomdhibiti katika himaya yake ndogo.

Amini usiamini, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa kimaumbile na mwingine na wala hatakuweko. Hata watoto pacha kutoka yai moja la mama hawawi sawa; lazima watatofautiana. Si nadra kusikia mtu amepata ajali akahitaji msaada wa damu na pakosekane kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kumwauni. Basi ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni.

**MASWALI**

a) Kwa nini mwandishi anadai kuwa maisha ya binadamu ni kioja kikubwa? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b) Kwa mujibu wa taarifa hii nini maana ya "..ngono... yenye ufanisi"? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

c) Uchunguzi wa sayansi umekita mizizi imani gain ya kidini? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

d) Thibitisha madai ya mwandishi kuwa kiumbe kilicho tumboni mwa mamake hawi katika "hali ya ukupe". (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

e) Toa sababu ya elimu ya kutoka kwa jamii na mazingira kuelekea kuwa bure ghali (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

f) " ………hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa na mwingine……." Kulingana na taarifa hii ni nini husababisha hali hii? Vipi? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

g) Eleza maana ya maneno au mafungu ya maneno yafuatayo.

(i) Himaya (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Kumwauni (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

2. **UFUPISHO**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu inaswali yanayofuata.**

Miili yetu hujengwa na chakula tulacho. Kila mara mwili wa mwanadamu hupoteza sehemu yake; kila kiungo kinapojimudu hutokwa na sehemu ndogo, na sehemu zile zinazotoka hurudishwa na chakula tulacho. Kila kiungo mwilini mwetu huhitaji sehemu ya chakula.

Ubongo hauna budi kupata sehemu yake; mifupa, misuli na neva pia zinahitaji sehemu zao. Ni kazi ya ajabu sana inayobadilisha chaküla kwa damu, na kutumia damu hii kwa kuvijenga viungo mbalimbali vya mwili; lakini kazi hii inaendelea daima, ikileta uzima na afya kwa kila neva, misuli na minofu.

Vyakula ambavyo vingechaguliwa kwa matumizi ni vile tu ambavyo vinahitàjiwa kwa kuujenga mwili. Maana yake, si kwamba inatupasa kuchaguà chakula kwa ajili ya utamu tu. Tamaa ya chakula ya watu wengi imepotoka kwa desturi mbaya za kula. Mara nyingi hutamani chakula kinachodhoofisha mwili na kuleta udhaifu badala ya nguvu. Si lazima tuongozwe na desturi za kikabila. Maradhi mengi na maumivu yanayoenea pote duniani hutokana na makosa ya wanadamu katika kuchagua chakula.

Nafaka, matunda, kokwa na mboga ndivyo vyakula tulivyochaguliwa na Muumba wetu. Vyakula hivi, vikiandaliwa vivi hivi, vinaleta afya mwilini na kututia nguvu. Vinamtia mwanadamu nguvu, uwezo wa kuishi miaka mingi, na akili timamu ambazo hazipatikani katika vyakula vilivyoungwa sana.

Lakini si kwamba vyakula vyote vilivyo na manufaa vinafaa mahitaji yetu katika hali zote. Ingetupasa kujihadhari sana katika kuvichagua vyakula. Chakulã chetu kingefuatana na hali ya majira, hali ya nchi tunapokaa, pamoja na kazi tunayoifanya. Vyakula vingine ambavyo vinaweza kutumiwa katika majira fulani ya mwaka na katika hali fulani ya nchi havifai kutumiwa kwa hali ya nchi nyingine, na katika majira mengine. Hivyo kuna vyakula maalum vinavyofaa kwa watu wanaofanya kazi ngumu za juhudi na havifai kutumiwa na watu wanaofanya kazi za afisini za kuketi na kufikiri. Mungu amtupa namna mbalimbali za vyakula vyenye kuleta afya, na inampasa kila mtu achague namna ya vyakula ambavyo kwa ujuzi wake ameviona kuwa vinafaa kwa mahitaji yake.

**MASWALI**

(a) Bila kupoteza maana fupisha yaliyomo katika aya mbili za kwanza za makala haya. (maneno 70)
(Mtiririko - alama 1) (alama 7)

**Nakala Chafu**

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………

..…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………..………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...……

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...……

……………………………………………………………………………………………………

**Nakala Safi**

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………

..…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………..………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...……

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...……

(b) Fupisha aya mbili za mwisho za taarifa hii. (Maneno 60-65)
Mtiririko (alama 1) (alama 6)

**Nakala Chafu**

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………

..…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………..………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...……
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………...……

**Nakala Safi**

……………………………………………………………………………………..
…..…………………………………………………………………………………………...
……..…………………………………………………………………………………………...
……….……………………………………………………………………………………
..……….……………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………...………………
………………..……………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………...……
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………...……

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Andika katika usemi wa taarifa.

“Ninataka kumwona mwanafunzi aliyehusika katika sakata hii sasa hivi!” Mwalimu Mkuu alisema. (alama 3)

……………………………………………………………………...……………………………….
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...………………………….

b) (i) Yakinisha sentensi ifuatayo:

Hasikii la mwadini wala la mteka maji wsikitini. (alama 1)

……………………………………………………………………...……………………………….
……………………………………………………………………………………………………………

(ii) Kanusha sentensi ifuatayo:

Analia tu akipigwa (alama 1)

……………………………………………………………………...……………………………….
……………………………………………………………………………………………………………

c) Eleza maana zozote tatu zinazowasilishwa na sentensi ifuatayo:

Mara tu alipofika, aliwekewa mikono. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

d) Onyesha mzizi wa kila kitenzi katika orodha ifuatayo.

(i) Hawajala (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

(ii) Sikumkuta (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

(iii) Walipiganishwa. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

e) Eleza matumizi mbalimbali ya "ni" katika sentensi ifuatayo:

Nendeni mkamwite Kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

f) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo

Mwalimu huyu anafundisha Kiswahili (Maliza kwa kiashiria kisisitizi) (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

g) Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo:

(i) Uhusiano wa zaidi ya hayo (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

(ii) Kuonyesha chanzo (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

h) Changanua sentensi ifuatayo kwa vistari/vishale

Kandanda ni mchezo maarufu duniani. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

i) Bainisha nomino zilizomo katika sentensi.

Ufisadi umeifilisi nchi ya Kenya. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

j) Unda nomino kutokana na nomino zifuatazo.

(i) Paka (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

(ii) Chuma (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

k) Andika kwa ukubwa

Simba aliingia katika nyumba na akafumwa mkuki. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

i) Taja sauti mbili zinazotolewa katika kaakaa laini (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

m) Bainisha shamirisho kipozi, kitondo na alalkitumizi katika sentensi ifuatayo:

Mwanafunzi alimbebea mwalimu runinga kwa toroli. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

n) Tunga sentensi ukitumia kuinganishi kifuatacho:

Maadamu (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

o) Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani?

(i) nyama. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) wema (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

p) Akifisha sentensi hii

Ah huu ndio mkutano aliotuitia mmoja wao aliropoka. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

4. **ISIMUJAMII**

(a) Fafanua nadharia tatu zinazoelezea kuhusu chimbuko la Kiswahili. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(b) Eleza njia saba za kuondoa baadhi ya matatizo yanayokumba lugha ya Kiswahili kwa sasa nchini Kenya. (alama 7)

*© 2010 Halmashuri ya Mtihani Wilaya ya Bureti* 

**MWISHO**